ISSN: 2320-5407 Int. J. Adv. Res. 10(05), 468-478

Journal Homepage: -www.journalijar.com

INTERNATIONAL JOURNAL OF ADVANCED RESEARCH (IJAR)

Article DOI:10.21474/IJAR01/14728
DOI URL: http://dx.doi.org/10.21474/IJAR01/14728

*RESEARCH ARTICLE*

# RIWAYA ZA KIMAJARIBIO; BURUDANI AU KIKWAZO KWA MSOMAJI? MFANO WA RIWAYA TEULE ZA K.W. WAMITILA

**Janice M. Mutua**
Chuo Kikuu Cha Egerton, Kenya.

## Manuscript Info

*Manuscript History*
Received: 15 March 2022
Final Accepted: 17 April 2022
Published: May 2022

*Key words:-*
Riwaya Za Kisasa, Riwaya Za Karne Ya 21, Muundo, Mtindo, Uandishi Bunifu, Hadhira

## Abstract

Makala hii imefafanua sababu za uchangamano wa muundo na mtindo wa riwaya za kisasa uliosababishwa na matumizi mapana ya mbinu za kimajaribio. Lengo mahususi lilikuwa kufafanua kuwepo kwa uandishi wa kimajaribio wenye kukanganya na athari zake kwa usomaji wa riwaya za kisasa. Japo kuna mitindo tofauti ya uandishi iliyozoeleka, mwandishi wa riwaya za kisasa hujikita katika ubunifu usiofuata mtindo mmoja maalum unaozifanya riwaya husika kuwa za kipekee. Makala hii imejibana katika ufafanuzi wa sababu za upekee wa riwaya hizo. Nadharia ya usasaleo imeuongoza mjadala huu katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Mintarafu ya nadharia, mwandishi bunifu ana uhuru wa kuandika jinsi apendavyo bila kufuata utaratibu fulani mahususi. Mkabala wa uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kuchanganua data iliyohusiana na swala zima la ubunifu wa riwaya mpya ya Kiswahili. Data ilichanganuliwa kwa kuangazia maudhui na vipengele kadha vya mbinu za kiuandishi za kimajaribio. Riwaya za kisasa za Mwandishi, Msomaji na Mwandishi na Msichana wa Mbalamwezizimetumika kuangazia mchakato huu. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Riwaya zimebaini kuwa sura na ubunifu wa riwaya mpya ni zao la usomi. Kwa hivyo, ili kuelewa ujumbe katika riwaya za kisasa ni muhimu kwa msomaji kufanya utafiti wa kina na kuwa na ufahamu wa mambo mengi kiada ili kung'amua yanayowasilishwa katika riwaya za kisasa.

*Copy Right, IJAR, 2022,. All rights reserved.*

## Introduction:-

Uandishi bunifu ni zoezi la kimantiki linalosababishwa na mwito wa kipekee wenye hisia kali zinazompitikia mwandishi akilini. Mwandishi mwenye hisia hizi hawezi kuzipuuza wala kujizuia kuyaandika mambo jinsi ayaonavyo na jinsi apendavyo.Kutofuata mitindo ya uandishi iliyozoeleka kumewapa wasomaji wa kisasa majukumu mengi ya kushughulikia kiada ili waelewe yale yanayowasilishwa na waandishi wa kisasa.Upande mwingine, katika mfumo wa mwanzo-kati-mwisho kazi ya fasihi huwasilishwa kwa njia ya moja kwa moja inayoegemea mtindo wa kihalisia. Mwamzandi (2013) anafafanua kwamba mtindo wa uandishi uliozingatia uhalisia ni mzuri ingawa kwa sasa unatiliwa shaka. Aidha, wasomaji wa fasihi ya sasa wako tayari kupokea kazi za kimajaribio kwa sababu wachapishaji wamezipa kazi hizo nafasi katika uchapishaji ingawa zina uchangamano.

Riwaya za kimajaribio ni aina ya riwaya inayojitokeza katika mikondo miwili: mkondo wa mjadala-nafsi na mkondo wa riwaya-kweli (Mulokozi, 1996).Watunzi wa riwaya za kimajaribio hupuuza umbo la kawaida la riwaya kwa



**Corresponding Author:- Janice M. Mutua**
Address:- Chuo Kikuu Cha Egerton, Kenya.

kuwa halitoshelezi mahitaji ya fasihi ya Karne hii ya Ishirini na Moja yenye maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano.Mtiririko wa visa na matukio unapokiukwa msomaji hujipata taabani. Utafiti huu umebaini kwamba itambidi msomaji wa kisasa ajihami na ufahamu wa mambo mengi ya kijamii, kisayansi, kiteknolojia, kisiasa miongoni mwa mengine kiada ili aelewe wayasemayo waandishi wa kisasa. Hii ni kwa sababu kazi za riwaya za kisasa zinachanganya mbinu za kijadi na za kisasa katika uandishi wake. Uhuru wa uchapishaji uliopo hivi leo umepelekea kuwepo kwa kazi nyingi mpya mpya za riwaya zenye sifa mpya za mbinu mpya za kiuandishi za kimajaribio. Je, riwaya za kisasa ni burudani au kikwazo kwa hadhira?Kujibu swali hili utafiti umeangazia uandishi wa mwandishi wa kisasa Kyallo Wadi Wamitila. Si kwamba huyu ndiye mwandishi wa pekee wa riwaya za kimajaribio ila ametumiwa kama kiwakilishi cha uwanda mzima wa uandishi wa kimajaribio.

**Mapitio ya Maandishi:-**

Sehemu hiiimeangazia historia ya riwaya ya kisasa. Kwa ufupi imebainisha mabadiliko ya aina aina yaliyoikumba riwaya iliyopo sasa ambayo ndiyo kiini cha utafiti huu. Utafiti umetalii maandishi kuhusu chanzo na ukuaji wa riwaya za kimajaribio. Sifa bainifu za riwaya za kimajaribio zimeangaziwa pia. Istilahi riwaya zakimajaribio, riwaya za kisasa na riwaya za Karne ya Ishirini na Moja zina maana sawa. Aidha, mwandishi wa kisasa ni sawa na mwandishi wa kimajaribio.

**Yaliyoandikwa kuhusu Chanzo na Ukuaji wa Riwaya za Kimajaribio:-**

Barth (1984) anasema kwamba kitovu cha uandishi wa kimajaribio ni mabara Uropa na Marekani ambapo uandishi wa kimajaribio ulihusishwa na enzi za usasaleo na uzinduzi wa kitaaluma. Katika kitabu chake Introduction to Literature of Exhaustion Barth anaeleza kwamba uandishi wa kimajaribio ulipata umaarufu mkubwa katika miaka ya 1910. Wazungu na Wamarekani walianza kwa kujaribu hali chache za uandishi wa kimajaribio. Hali zilizotumika sana katika utunzi wakati huo ni matumizi ya vijikaratasi-chapwa na vihadithi vidogo vidogo. Waandishi wa kazi za nathari zilizovuma wakati huo ni pamoja na T.S. Eliot na Gertrude Stein. Riwaya Ullysses ya mwandishi James Joyce iliandikwa na kuchapishwa wakati huo.Ni dhahiri kuwa ingawa uandishi wa kimajaribio umekuwepo tangu jadi ila sasa umekumbwa na mabadiliko kila uchao. Vipindi tofauti tofauti vya historia vilichangia katika mabadiliko ya kimuundo ya riwaya.

Mchango mkubwa katika maendeleo na ukuaji wa riwaya za kimajaribio ulitokea katika kipindi cha historia cha Avant-garde(Kneppert na Deckard, 2016).Uandishi huu wa kimajaribio ulichochewa na hali za kisiasa zilizokuwepo wakati huo ambapo wanajamii walitaka uhuru, haki na usawa katika nyanja zote za jamii zao, uandishi ukiwemo. Kipindi cha Avant-garde kilifuatwa na vuguvugu jingine lililojiita Dada lililoibuka na kusisitiza kuwepo kwa uandishi wenye uhuru wa kuwasilisha mawazo (Barth, 1984). Kwa hamasisho hili mwandishi Tristan Tzara alitumia uhuru wa utunzi kuandikia manifesto yake iliyosisimua. Kwa kutumia vijikaratasi vyenye matini tofauti tofauti alizokata kutoka kwenye magazeti na kuzifanya nyenzo za kuwasilishia manifesto hiyo, Tzara aliamsha ari mpya ya ubunifu ambao umeendelezwa katika Karne ya Ishirini na Moja na matumizi ya urejeleomatini katika riwaya.

Kwa mujibu wa Barth (1984), katika miaka ya 1910-1920 kundi jingine la kimapinduzi, The Surrealist Movement lilitumia mbinu zilizokiuka kaida na utaalamu wa kijadi ili kuamsha hisia za jamii na kuihamasisha kwa uandishi bunifu. Katika miaka ya 1960 ilibainika wazi kuwa utukufu wa usasa ulikuwa umekita mizizi na kudidimiza usasaleo katika maswala ya uandishi. Uandishi na uchapishaji wa bunilizi za kimajaribio ulipungua kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, ukakamavu wa mwandishi William Burrough katika riwaya Naked Lunch uliibua hisia nzito za hamu ya kuwa na uhuru katika uandishi. Katika uhuru huo, Burrough aliibua mbinu mpya iliyoitwa “Cut-up” ambapo matini zilizopigwa chapa zilikatwa kutoka magazetini na vitabu vingine na kutumika katika uandishi wa riwaya (Barth, 1984). Umaarufu wa uandishi wa kimajaribio uliwafanya waandishi wa kihalisia kama Bernard Malamud na Norman Mailer kuukumbatia. Sifa bainifu ya kimajaribio iliyotumika zaidi katika uandishi ni matumizi ya bunilizi ndogo ndogo zilizotapakaa katika bunilizi kuu. Msanii mwengine aliyebobea wakati huo alikuwa Thomas Pynchon. Aliandika riwaya Gravity’s Rainbow iliyonunuliwa kwa wingi sana. Maelezo ya Barth yanabaini kuwa uandishi wa kimajaribio uliongeza elementi mpya za uandishi kulingana na mpito wa wakati.

Martha (2008) ametafiti kuhusu riwaya za kimajaribio kati ya miaka ya 1970 – 1980. Kwa mujibu wa utafiti wake riwaya za nyakati hizo zilikuwa na sifa za kimajaribio zilizokuwa changamano zaidi. Akirejelea riwaya If on a Winter’s Night a Traveller ya Italo Calvino,Martha anasema kuwa riwaya yenyewe ilikuwa changamano katika mpangilio wa sura. Baadaye katika mwaka 2005 waandishi wapya wa kimajaribio waliibuka. Hao ni pamoja na Juan Rulfo wa Mexico katika Pedro Paramo, Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia katikaOne Hundred Years of

Solitude, Mario Vargas wa Peru katika The War of the End of the World, Giannina Braschi wa Puerto Rico katikaYo-Yo Boing na Lezanna Lima wa Cuba katika Paradise (Barth, 1984).

Katika Karne ya Ishirini na Moja riwaya za kimajaribio zilihusiana na kuibuka kwa matumizi ya tarakilishi na teknolojia za kidijitali. Elliot (2017) katika ufafanuzi wa riwaya Z213:Exit ya Dimitris Lyacos anafafanua kuwa ni hadithi iliyoandikwa kwa kurejelea simulizi nyingi fupi fupi. Riwaya ya Dimitris ni hadithi nzuri lakini uchangamano wa mtindo na msuko wake huweza kumchosha msomaji (Elliot, 2017). Kwa misingi hii utafiti huu ulizingatia jinsi mwandishi K.W. Wamitila anavyopanga na kutumia kipengele cha bunilizi nyingi fupi fupi katika riwaya kuu katika uwasilishaji wa ujumbe wake kwa jamii. Aidha, mtafiti amejadili athari za tendo la uchupaji wa vihadithi vidogo vidogo katika hadithi kuu.

Mbinu za kiuandishi za kimajaribio zilikita mizizi barani Afrika kwa mara ya kwanza kwa uandishi wa riwaya katika lugha ya Kiingereza (Zabus, 1997). Uandishi wa riwaya ya Things Fall Apart ya Chinua Achebe mnamo mwaka 1958 ulisisimua ari ya waandishi wengine wa Kiafrika. Katika mwaka wa 1973, Ayi Kwei Armah aliandika riwaya ya Two Thousand Seasons hukuEmecheta Buchi akiandika The Slave Girl mnamo mwaka 1977.Riwaya iliyokuwa na mabadiliko makubwa zaidi ya kimajaribio barani Afrika wakati huo ilikuwa Sozaboy ya Ken Saro-Wiwa. Mwandishi huyu alikiuka sheria ya kijadi ya utunzi kwa kutumia lugha yenye makosa mengi ya kisarufi ili kuonyesha uozo uliokuwa katika nchi ya Nigeria wakati huo. Maovu ya dhuluma na ufisadi yalikithiri nchini humo. Riwaya yenyewe ilifahamika kama, "A Novel in Rotten English" (Zabus, 1997). Kwa misingi hii utafiti huu ulifafanua matumizi ya lugha huru ambayo ni mojawapo ya sifa bainifu za kimajaribio. Mtafiti ameonyesha jinsi riwaya zilivyotumia lugha huru kuyafichua maswala mbalimbali ya kindani yaliyofichika katika jamii husika.

Wakirejelea uandishi wa kimajribio barani Afrika, Deleuze na Guattari (1986:26) wanasema kuwa riwaya za Kiafrika zilifanyika kuwa "fasihi ya wachache iliyoandikwa kwa lugha ya wengi". Katika utambuzi na ufafanuzi wa mbinu za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya teule za kisasa, utafiti huu ulichanganua matumizi ya lugha huru kama kipengele cha uandishi wa kimajaribio. Uchanganuzi wa lugha iliyotumika umethibitisha ukweli wa usemi kuwa "riwaya mpya imefanyika kuwa fasihi ya wachache iliyoandikwa katika lugha ya wengi". Zaidi ya haya, Barani Afrika Khamis (1998) anaeleza kuwa mabadiliko mengine katika riwaya ya Kiswahili yalianza kushuhudiwa kuanzia miaka ya 1990 kwa uchapishaji wa riwaya za Euphrase Kezilahabi; Nagona na Mzingile mtawalia.Gromov (1998) anaendeleza kauli kuwa riwaya za Kezilahabi zilikiuka kabisa kaida za utunzi wa bunilizi za kijadi za Kiswahili. Badala ya mtindo wa kijadi, ziliegemea mtindo wa uhalisia-mpya. Zilionyesha sifa bainifu za kimajaribio katika fani za muundo na mtindo. Tangu wakati huo riwaya za Kiswahili za kimajaribio zimeandikwa na kuchapishwa kwa wingi hasa nchini Kenya na hali kadhalika kwingineko katika Afrika Mashariki. Tofauti na tafiti zilizotajwa, utafiti huu ulichanganua vipengele, mitindo na miundo ya kimajaribio iliyotumika katika riwaya za kisasa zikiwakilishwa na riwaya mbili teule zilizoandikwa na K.W. Wamitila. Uchangamano uliopo katika riwaya za kimajaribio umezifanya riwaya hizo kukosa kutimiza lile jukumu la fasihi la kuburudisha.


**Mbinu Za Utaftii:-**

Utafiti huu ulikuwa wa kithamano uliojiegemeza katika mkabala wa kifasili. Matokeo yalitolewa kwa njia ya kimaelezo kwa kuwa deta iliyotumika haikuwa ya kitakwimu. Kwa mujibu wa Creswell (2009) katika Maree (2012) deta isiyo ya kitakwimu huelezwa kwa maneno. Kwa kuzingatia udurusu wa yaliyomo, mtafiti alitambulisha mbinu mbali mbali za kimajaribio alizotumia mwandishi wa riwaya teule kuwasilishia ujumbe wake kwa jamii. Kwa kuwa utafiti huu ulihusu jinsi mitindo ya kimajaribio katika fasihi ya kisasa inavyowasilisha maudhui yanayoiakisi jamii husika, sifa za mbinu zilizotumika zimejitokeza katika fani za kiutunzi kama vile usimulizi, lugha, wahusika, muundo na hali kadhalika msuko wa kazi husika (Neuendorf, 2002).

Utafiti huu unahusisha sehemu au sampuli ndogo ya riwaya za kisasa zilizoandikwa na mwandishi wa kisasa, Kyallo Wadi Wamitila. Si kwamba huyu ndiye mwandishi wa kimajaribio peke yake ila ameteuliwa kama kiwakilishi cha idadi kubwa ya waandishi wengine wa kimajaribio. Vile vile, sampuli ya riwaya tatu za mwandishi zilizohusishwa katika utafiti ambazo zilichaguliwa kwa njia ya kimakusudi pia ni kiwakilishi cha riwaya nyingine za kimajaribio alizoandika mwandishi Wamitila. Sifa zilizoongoza uteuzi wa riwaya zilizotumika katika utafiti ni ujidhihirishaji wa uandishi wa kimajaribio ambao sifa yake kuu ni ukatizwaji wa masimulizi. Kwa mujibu wa Dalen (1979) sehemu ndogo ya idadi lengwa inapochaguliwa hufanyika kuwa kiwakilishi tosha katika zoezi la ukusanyaji na uchanganuzi wa deta kutoka kwa jamii pana. Kama ilivyotajwa awali, si riwaya hizi pekee zilizo na sifa za kimajaribio bali zimeteuliwa kuwakilisha kundi zima la riwaya za kimajaribio kama wanavyodokeza Mugenda na Mugenda (2003) kwamba;

Hamna sampuli inayoweza kuwa bora zaidi kuliko nyingine (tafsiri yangu).

Mchoro ufuatao unaonyesha mpango maalum wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data.




**Kielelezo 1:-** Muundo wa Mpango Maalum wa Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Deta.

**Matokeo na Muhtasari:-**
Riwaya za kisasa zimekuwa ngumu kueleweka na msomaji kwa sababu ya kukosa usimulizi wa moja moja au uhalisia. Riwaya husika ni changamano. Uchangamano wake unasababishwa na ukatizwaji wa usimulizi. Mbinu tofauti tofauti za utunzi wa kimajaribio zimechangia pakubwa katika ukatizwaji wa usimulizi unaopelekea uchangamano uliopo katika riwaya za kisasa.

Mbinu ya kimajaribio iliyotamalaki katika riwaya teule zilizotafitiwa ni matumizi ya muundo changamano ambao umepelekea kuwepo kwa ukatizwaji wa usimulizi. Ukatizwaji wa usimulizi umejidhihirisha katika mitindo na miundo mbali mbali ya usimulizi iliyotumiwa katika riwaya teule. Vile vile, ukatizwaji wa usimulizi umechangiwa na matumizi ya mbinu nyingi za sanaa na lugha zilizotapakaa kote riwayani. Ukatizwaji wa usimulizi ni hali ambapo mwandishi anazungumzia jambo fulani kisha kabla ya kulikamilisha akaliacha na ghafla akaanza kuzungumzia jingine. Usimulizi wa aina hii umekithiri katika riwaya teule. Aidha, ni aina ya usimulizi ambao umeathiri riwaya za kimajaribio kwa kuzifanya kukosa mtagusano wa kifasihi uliozoeleka. Mbinu mbali mbali za kimajaribio zimetumika katika kuujenga ukatizwaji huu wa usimulizi. Kando na kukatiza usimulizi, riwaya husika zimetumia mbinu hizo kuwasilisha maudhui na kutoa taswira kamili ya jamii ya kisasa. Taswira kamili ya jamii ya kisasa inayojidhihirisha kwa jumla ni kwamba ni jamii isiyopendelea kufuata utaratibu. Ni jamii inayofahamu mengi ambayo inayawasilisha kwa pamoja pasina kufuata mpangilio wowote.

Ukatizwaji wa usimulizi umebainika kila uchao katika riwaya teule. Ujenzi wake umejitokeza katika vipengele mbali mbali vilivyodhihirika katika utunzi wa kimajaribio. Vipengele hivyo vimerejelewa katika utafiti huu kama sifa bainifu za mbinu za kiuandishi za kimajaribio. Vipengele vilivyobainishwa vimejitokeza katika simulizi fupi fupi zilizotapakaa katika usimulizi mkuu wa kila riwaya iliyoteuliwa. Vipengele hivi ni pamoja na; urejeleomatini, taashira, uhalisiajabu na mwingilianotanzu. Uandishi wa kimajaribio unawiana na maoni ya Lyotard (1984) kwamba riwaya haiwezi kuwa na mpangilio wa moja kwa moja kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa sababu hii ukosefu wa mpangilio wa moja kwa moja umesababisha uchangamano mpana katika ploti na usimulizi kwa jumla katika riwaya teule (Rettova, 2016). Hata hivyo, mwandishi amefanikiwa katika kuwasilisha ujumbe muhimu kuhusu maswala yanayoikabili jamii. Vile vile amefanikiwa kuichora taswira kamili ya jamii ya leo kwa kutumia mbinu za kimajaribio. Kuna utofauti wa jinsi kila mbinu inavyodhihirisha ukatizwaji wa usimulizi unaounda muundo changamano ambao ndio nyenzo kuu ya uandishi wa kimajaribio katika kila riwaya. Mbinu zilizochangia katika ukatizwaji wa masimulizi katika riwaya teule ni simulizi fupi, urejeleomatini, uhalisiajabu na mwingilianotanzu. Mbinu husika zote zimedhihirika katika simulizi fupi fupi. Matumizi yake yamezifanya riwaya za kimajaribio kuwa kikwazo kwa wasomaji.

**Simulizi Fupi:-**

Simulizi fupi zinapochupwa kote katika usimulizi husababisha riwaya yenye muundo changamano. Simulizi fupi katika riwaya iliyobuniwa kwa kufuata mtindo na muundo mgumu huendeleza ukatizwaji wa usimulizi katika riwaya nzima na hivyo kuifanya kuwa na ugumu wa kufuatiliza matukio (Abrams, 1993). Aidha, muundo wariwaya hii huwa ni kinyume cha muundo sahili ambapo uwasilishaji wa riwaya huwa ni wa moja kwa moja. Riwaya ya aina hii huhitaji umakini mwingi inaposomwa ili ieleweke. Sifa nyingine za riwaya zenye muundo changamano ni msuko tata, maudhui mengi, taharuki, taashira, matumizi mapana ya mbinu rejeshi/visengere nyuma na mbele pamoja na kuchanganya mtiririko wa mawazo. Katika riwaya teule uchangamano umedhihirika katika mchanganyiko wa miundo na mitindo mbali mbali ya msuko wa hadithi inayojitokeza katika takriban riwaya nzima. Muundo msago ambapo visa na matukio hupangwa katika hali ya kufuatana kuanzia mwanzo hadi mwisho umechanganywa na muundo rukia. Katika muundo rukia visa viwili au zaidi vimerukiana katika usimulizi wake lakini mwishoni vimeungana na kufanyika kuwa kisa kimoja. Muundo changamano ulioshuhudiwa katika riwaya teule umedhihirika katika miundo msago na rukia ambayo imetumika pamoja katika hadithi husika. Visa vimeanza kwa urejeshi na kumalizika kwa njia ya msago. Vile vile pameshuhudiwa kuwepo kwa masimulizi ndani ya masimulizi mengine. Tanzu tofauti tofauti za fasihi kama vile ngano, ushairi na fasihi simulizi pia zimeshuhudiwa katika riwaya zilizochunguzwa. Kuwepo kwa uchangamano katika riwaya mpya kumetatiza upokeaji na uelewekaji wa riwaya mpya. Vile vile uchangamano umebainika pale ambapo matini zimeingiliana, kuathiriana na kutegemeana ili kujenga riwaya mpya. Ndani ya simulizi fupi zilizotumika katika riwaya teule mna matumizi ya fani za fasihi kama vile taashira nyingi, dayolojia na uchanganyaji wa lugha. Taashira, dayolojia na uchanganyaji wa lugha zimejidhihirisha kama sifa bainifu za mbinu ya kimajaribio katika simulizi fupi kama katika mfano huu.

Ninaota siku moja kuiandika riwaya. Na sio riwaya tu lakini riwaya mahususi ambayo haitakaa tu isomwe bali itasaidia usomaji wake **(ML UK.2).**

Kwa kutumia simulizi fupi mwandishi anadai kuwa angependa kuiandika riwaya mpya ambayo ingejisoma yenyewe. Katika simulizi hii, taashira "kujisoma yenyewe" imetumiwa kudhihirisha kwamba hadithi husika itakuwa kioo halisi cha jamii inayorejelewa. Ili jamii ifahamike, mwandishi bunifu atahitajika kukubali msukumo usiozuilika wa uandishi ili ndoto yake ya kuionyesha jamii yake kwa nyingine itimizwe. Katika simulizi fupi hii, mwandishi anaendelea kusema kuwa hadithi atakayoitunga itaitwa Musaleo. Katika muktadha unaorejelewa, “Musaleo” ni ufupisho wa “Musa wa leo” yaani mkombozi wa leo. Matini ya kidini hii ya kidini imetumika kuleta kumbukumbu ya kiongozi wa kabila la Israeli aliyefahamika kama Musa. Katika dini ya Kikristo, imerekodiwa katika Biblia kitabu cha Kutoka kuwa Musa alikuwa mkombozi wa wana wa Israeli. Inaaminika katika dini hiyo kwamba Musa alitumwa na Mungu kuwakomboa Waisraleli kutoka utumwani Misri walikotumikishwa na Firauni. Hivyo ndivyo alivyofanyika kuwa mkombozi. Vivyo hivyo, inabainika kuwa baadhi ya mataifa ya Kiafrika yanayoendelea yanahitaji mkombozi wa kuyatoa katika utumwa wa maovu yanayoyakumba. Baadhi ya maovu husika ni kama vile njaa, mauaji na ufisadi unaosababishwa na matumizi mabaya ya mamlaka. Mintarafu ya haya, riwaya mpya itajisoma yenyewe kwa kuibaini taswira hii ya jamii ya kisasa, matatizo yake na mapendekezo kuhusu ukombozi wake. Aidha, inatarajiwa kuwa “Musa wa leo” ataikomboa jamii kutokana na uongozi dhalimu miongoni mwa matatizo mengine. Matumizi ya mbinu hizo zote kwa pamoja huweza kumkanganya msomaji anapojaribu kung’amua anayosema mtunzi.

**Taashira:-**

Taashira ni neno lenye asili yake katika Ugiriki ambapo lilitumika kwa maana ya kubadili jina (Myers na Simms, 1989). Tamathali hii hutumia neno au fungu la maneno badala ya neno au fungu jingine la maneno. Hivi ni kusema kwamba neno au fungu la maneno la kinachozungumziwa husimamia kitu kingine au maana nyingine. Mwakio (2014) anaendeleza hoja hii kwa kueleza kuwa taashira ni matumizi ya lugha ya ishara kwa minajili ya kuwakilisha na kuwasilisha ujumbe fulani. Mwakio anaendelea kusema kuwa jina, tukio, jambo au kitu fulani hutumika kumaanisha kitu kingine chenye uhusiano na kile kilichotumiwa. Majina, vitu au hali fulani zinazotumika kama taashira huwa zinafahamika vizuri katika jamii kwa jumla kuwa na uhusiano wa karibu na hali zinazowakilisha. Kwa mujibu wa Senkoro (1982), mwandishi wa kazi za fasihi hurejelea sifa na tabia za watu na vitu mbalimbali kwa kusudi la kuashiria mambo fulani mahususi yanayoendelea katika jamii anamoandikia.

Akimnukuu Senkoro (1982) Mwakio (2014) anafafanua kuwa taashira kama tamathali ya lugha huchukua jina la kitu kidogo kinachohusiana na kingine kikubwa na kukitumia katika uandishi ili kuwakilisha kitu fulani kamili. Maoni haya aidha yameendelezwa na wataalamu Mbatiah (2001) na Karanja (2014). Kwa upande wake, William (2003) anaeleza kuwa neno au fungu la maneno linalotumiwa kama taashira halina maana mahususi ya moja kwa moja bali huzua maana nyingi kulingana na muktadha uliotumiwa. Karanja (2014) anasisitiza kwamba neno au fungu la maneno linalosimama badala ya neno au fungu jingine sharti liwe na uhusiano fulani wa kimaumbile, kisifa, kisemantiki au uhusiano mwingine wowote ule na kile kinachoashiriwa. Ufafanuzi wa Leech (1969) unatambulisha kuwa dhima ya taashira katika utunzi ni kuleta maana ya kibunifu ambayo huwa imehamishwa kutoka kwa kitu cha kawaida kama kinavyofahamika na jamii. Kwa mujibu wa maelezo haya ni bayana kuwa taashira hutumika katika bunilizi kuwakilisha maana iliyofichwa katika vitu, hali au mambo ya kawaida. Kuna aina tofauti tofauti za taashira kama inavyodhihirika katika maelezo ya Frye et al. (1993). Wanaeleza kuwa taashira hujidhihirisha katika aina tatu yaani sinekidoki, taniaba na lakabu. Mfano mmoja wa taashira iliyotumika katika riwaya husika ni kama ifuatavyo;

“Akakumbuka hata visa alivyofundisha mwenyewe alipokuwa shuleni: kule **giza** linatamalaki; **wenyeji na wala watu**”.

Giza ni hali ya ukosefu wa mwangaza au nuru. Palipo na giza binadamu hawezi kuona mbele. Katika nukuu hili bara la Afrika linafananishwa na giza. Linaitwa bara lenye “wenyeji wala watu”. Katika enzi za ukoloni nchi za Afrika hazikuwa na maendeleo kama walivyodai wakoloni (Pakenham, 1992). Dhana giza imetumika kama taashira kuikumbusha hadhira sura ya Afrika kabla ya majilio ya wazungu. Wazungu wakoloni walidai kuwa walikuja Afrika ili kuwaondoa wenyeji katika hiyo giza. Mwandishi kwa kutumia sifa ya taashira anaichorea hadhira yake taswira ya Afrika kabla ya utawala wa kikoloni. Hata hivyo, Waafrika wenyewe waliridhika na kufurahia jinsi walivyoishi hata ingawa wazungu waliowaona wakiwa gizani. Giza imetumika kama hali inayotetemesha na kutamausha.

**Dayolojia:-**

Asili ya neno dayolojia ni maneno mawili ya Kigiriki “dia” lenye maana ya “kati ya” na “logos” lenye maana ya “zungumza” (Jazdzewska, 2015). Hivyo, dayolojia ni mazungumzo kati ya watu (wahusika) wawili au zaidi kuhusu jambo fulani. Mazungumzo yanaweza kuwa ya ana kwa ana, kwa njia ya simu au kwa maandishi. Kwa maneno mengine, dayolojia ni mazungumzo au majibizano baina ya watu wawili au zaidi wakiwa katika hali ya kupokezana maneno. Katika fasihi andishi dayolojia au mazungumzo hupitishwa kwa njia ya kimaandishi. Katika riwaya teule dayolojia zimechukua miundo na mitindo tofauti tofauti. Japo mitindo hiyo ni tofauti, mazungumzo yalinuia kuendeleza msuko na mtindo wa usimulizi ulioishia kuwa changamano. Fauka ya haya, dayolojia zimetumika kukuza wahusika, kufafanua mandhari na mazingira ya usimulizi pamoja na kukuza ufaafu wa mbinu ya kimajaribio ya simulizi fupi katika juhudi za kuiakisi jamii ya leo. Katika riwaya teule, dayolojia zimeendelezwa kwa kutumia sentensi fupi fupi zenye vinukuzi.

Mtindo mwingine wa dayolojia katika riwaya teule ni mazungumzo mafupi ila yaliyotumika kwa wingi pamoja na fani na mbinu nyingine za lugha. Dayolojia zenye mtindo huu zimechanganywa na mbinu ya uchanganyaji wa lugha na kuwasilishwa kwa kutumia vinukuzi. Katika dayolojia husika mwandishi anayaangazia masaibu ya wananchi. Hii ndiyo taswira kamili ya jamii ya msimulizi. Dayolojia nyingine zimechukua mtindo wa kitamthilia ambapo mwandishi ananukuu maneno ya msemaji halafu anayaweka maelezo katika mabano. Mwandishi ametumia mtindo huu kuwasilisha maongezi ya wahusika. Musokile (1993) anaeleza kwamba katika dayolojia bunifu mwandishi au mtunzi huwa mhusika. Katika riwaya husika mwandishi ametafakari kwa makini mada anayolenga kuandikia

dayolojia kisha akatayarisha na kupanga mawazo kimantiki. Mawazo hayo ni sharti yapangwe kwa mtiririko bora. Hatimaye, mwandishi huwaunda wahusika na kuwapangia majukumu kulingana na matendo yao (Musokile, 1993). Mfano wa dayolojia ni kama ifuatavyo;

"Sasa vuka mto huu wewe na kijana. Mimi sasa siwezi, anayeweza ni Mamanchi na Kijana. Ng'ambo ya pili kuna njia inayopita karibu na mapango. Sehemu yenyewe in giza lakini usiogope. Hakuna giza lisilochewa".

Atakayeliondoa taifa na jamii ya sasa kutoka kwenye kilindi cha usumbufu ni mwanajamii mwenyewe. Japo kutakuwa na vikwazo vingi, bidi na ujasiri vitamwezesha kuleta tumaini jipya na tabasamu. Kwa kusema, "hakuna giza lisilochewa", mwandishi anadhihirisha kwamba hakuna tatizo lisilokuwa na mwisho. Dhuluma, madhila na shida zote katika jamii ya sasa ni nyingi na zinaumiza hisia, nafsi na mioyo lakini zina mwisho. Kwa maneno haya mwandishi anaipa jamii ya sasa tumaini la kupata maisha mazri mradi iwe na ujasiri wa kukabiliana na hali zinazoidhulumu kwa lengo la kupata suluhu la kudumu. Zaidi ya haya, ni dhahiri kwamba kuna ng'ambo ya pili iliyojawa na furaha ambayo kila mwanajamii anafaa kuitazamia.

**Uchanganyaji wa Lugha:-**

Simulizi fupi pia zimetumika pamoja na uchanganyaji wa lugha. Hii ni mbinu ya kutumia lugha mbili au zaidi kwa pamoja katika utungo mmoja. Lugha zaidi ya moja zinapotumika katika kazi yoyote husababisha athari tofauti tofauti. Sababu mbali mbali huwapelekea waandishi kuchanganya lugha au msimbo katika uwasilishaji wa kazi katika lugha ya Kiswahili.

a. Richards (1984) anasema kwamba ubadilishaji wa msimbo hufanyika ili kumsaidia msimulizi au mwandishi kujieleza vizuri kwa kufidia upungufu wa msamiati. Upungufu hutokana na mwandishi au msimulizi mwenyewe kukosa msamiati wa kutosha au kuwa katika hali kwamba lugha anayotumia hukosa msamiati wa kumtosha kuwasilishia ujumbe anaokusudia. Aidha, uchanganyaji lugha humsaidia mwandishi kuwasilisha hisia alizo nazo ambazo huenda zikawa za furaha, kirafiki au za kuchukiza. Katika kitengo hiki uchanganyaji wa lugha pia hutumiwa kutambulisha kundi fulani la waja kwa mfano vijana, madaktari, wasomi na wengine. Hali ya mwandishi kuwa na umahiri wa lugha moja zaidi ya nyingine pia husababisha ubadilishaji wa msimbo. Katika jamii lugha moja yaweza kuwa na hadhi kuliko nyingine (Chiraghdin na Mnyampala, 1977). Hapa watu hupenda kuchanganya au kubadili msimbo ili kujinasibisha na hadhi ya juu;
b. Sajili za miktadha mbali mbali pia husababisha ubadilishaji wa msimbo. Sajili ni vilugha ambavyo hutokana na tofauti za kikazi, eneo la makazi, urafiki wa karibu, umri au tabaka (Wardhaugh, 1986). Sajili hutekeleza majukumu kadha katika kazi bunifu kama vile: kurahisisha mawasiliano kwa lengo la kuelewana, kuhifadhi kumbukumbu, kuzungumza kwa kifupi na kuyatenga makundi yasiyo uhusiano na kundi husika;
c. Kuchanganya lugha humwezesha mwandishi kuficha siri zake kwa kuwatenga wasioelewa lugha anayotumia. Aidha, humsaida katika kudumu ndani ya mada anayoshughulikia kikamilifu. Mfano;

"Inavyoelekea …mmm…ana tatizo la brain tumour…au hata intracranial hypertension…! Ikiwa diagnosis yangu ni sawa kwa sababu sijawahi kukosea katika miaka yote hii niliyofanya kazi ya udaktari, ana siku kama ishirini na nane za kuishi…in fact it might even be less!"

Ujuzi wa kitaaluma umetumiwa kumdhulumu Yosi kimawazo na kihisia badala ya kutumika kumpa matibabu yafaayo. Ni dhuluma kwa sababu daktari anatoa uamuzi wa kutamausha kabla ya uchunguzi wa kimatibabu kufanywa. Baadaye kabisa, picha za uyoka zilipopigwa ilibainika kuwa Yosi alikuwa buheri wa afya. Daktari husika alikuwa amejigamba jinsi alivyokuwa mtaalamu aliyesomea udaktari katika vyuo-tajika, "alumnus wa prestigious universities", Hivyo, alipozungumza kuhusu hali ya mgonjwa wake, Yosi alijua na kuamini ukweli kwamba siku zake duniani zilikuwa zimefikia ukingoni. Kuna umuhimu wa kuchunguza jinsi masomo yanavyoendeshwa katika vyuo vikuu. Visibakie kuwa vyuo tajika tu na "alumnus" wake hawawezi kuifaa jamii katika mambo yawategemeayo zaidi kama afya. Ni hali ya kusikitisha kuona kwamba katika mataifa yanayoendelea hali ya afya inazidi kudorora licha ya kuwa na madaktari wengi waliohitimu katika vyuo tajika. Sababu zinazoyafanya mataifa yanayoendelea kuamini na kutafuta matibabu ya magonjwa sugu kama kansa Ughaibuni zimefafanuliwa. Kuna uwezekano kwamba ni kwa sababu ya ukosefu wa maarifa miongoni mwa madaktari wa nchi husika. Suluhu ni kuwa iwapo mitalaa ya masomo vyuoni itafumwa vizuri na sera ziangaziwe ifaavyo, mataifa ya Afrika yataweza kujitibu na kujiinua kiafya na pia kiuchumi.

**Urejeleomatini:-**

Urejeleomatini ni tafsiri ya neno la Kiingereza "intertexuality" lililotumika kwa mara ya kwanza na mwanafalsafa mfaransa, Julia Kristeva katika kitabu chake cha 'Dialogue and Novel'. Kwa mujibu wa Kristeva (1980), kila neno ni urejeleo wa maneno mengine. Hivyo, kuna msisitizo kwamba matini huhusiana na kutegemeana ili kuleta maana. Stam (2000) katika Anderson (2000:1) ananukuliwa,

"Matini yoyote ile iibukayo lazima iwe imelala pamoja na nyingine au na matini nyingine ambayo ile ya awali imelala nayo".

Usemi huu unadhihirisha kuwa kazi ya fasihi iliyotafitiwa haikutoka kwenye akili ya mtunzi pekee au katika ombwe tupu bali ni mkusanyiko wa matini nyingine tofauti tofauti. (Anderson, 2000) anadai kuwa urejeleomatini huhusisha " yale yaliyosemwa tayari". Urejeleomatini ni kipengele muhimu cha usasaleo ambamo mwandishi wa kisasa anatumia kuandikia kazi yake. Hivyo, urejeleomatini ni mojawapo wa elementi au mbinu kuu ya uandishi wa kimajaribio. Katika riwaya teule matini zimebainika katika simulizi fupi fupi, tanzu za fasihi simulizi zilizotumika na maoni ya wanafalsafa. Nyingine zimewasilishwa kwa matumizi ya uchanganyaji wa lugha.

Enani (2005) anadai kwamba urejeleomatini huathiri namna ya usomaji wa matini mpya hasa unapokuwa mwingi na wenye mitindo tofauti tofauti. Riwaya teulezimethibitisha kuwepo kwa urejeleomatini wakimtindo. Vipande vingi vilivyorejelewa katika riwaya teule vimeathiri msuko na ploti katika riwaya za kisasa. Hadhira (msomaji) inatiliwa huko na kutolewa kule. Msomaji anasoma kipande cha hadithi kilicho na matini rejelewa na kabla ya kukikamilisha kingine kinaanzishwa. Mbinu hii ya uandishi inachangia pakubwa katika kuleta uchangamano katika riwaya husika hivyo kuukatiza usimulizi. Wamitila (2010) anadai kuwa urejeleo wa aina hii waweza kuzua kuwepo kwa kazi hasi au chanya. Utafiti huu umebaini kuwa urejeleomatini ni kisababishi cha uchangamano katika riwaya za kimajaribio na kupendekeza mbinu za kuukabili.

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981:271) yale ambayo mwandishi wa kisasa anayasema ni zaidi ya matamko yenyewe. Hii ni kwa sababu miktadha mbalimbali huathiri kazi ya fasihi kwa njia tofauti. Miktadha kama ya kiuchumi, kijamii au kisiasa huathiri mahusiano fulani katika kazi za fasihi (Wamitila, 2010). Kwa mujibu wa haya, uchanganuzi huu umetambulisha aina za miktadha tofauti tofauti iliyorejelewa katika riwaya teule, mahusiano yake na jinsi inavyochangia katika uwasilishaji wa maudhui. Kupitia kwa mbinu ya kimajaribio ya urejeleomatini, mwandishi amefanikiwa kubainisha shughuli, imani na tabia za jamii anamoandikia. Hivyo, taswira kamili ya jamii imebainishwa kwa kuangazia mambo ya aina aina yanayojidhihirisha katika jamii husika kupitia kwa matini zilizorejelewa na mtunzi. Maudhui yaliyowasilishwa kwa kuzingatia kipengele cha urejeleomatini ni pamoja na dhuluma, utabaka, dini, maisha ya jamii, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana, uongozi na mahusiano mengine katika jamii. Isitoshe, kipengele cha urejeleomatini kimetumika kubaini chanzo cha uozo uliomo katika jamii ya sasa kwa jumla.

Uhalisiajabu pia hufahamika kama uhalisimazingaombwe. Asili ya dhana ya uhalisiajabu katika sana ni mnamo mwaka 1920 katika kazi za bunilizi za Jorge Luis Borges wa nchi ya Argentina (Faris na Zamora, 1995). Waandishi wengine wa kimajaribio waliobobea katika matumizi ya uhalisiajabu katika bunilizi zao za kinathari walikuwa Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, Isabel Alende wa Chile, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia na John Fowles wa Uingereza (Abrams, 1999). Waandishi wanaotumia uhalisajabu katika kazi ya fasihi husuka uhalisia pamoja na uhalisiajabu kwa njia maalumu inayobadilika badilika kwa lengo la kuwasilisha matukioa ya kihalisia na maelezo ya kina kwa njia ya kifantasia au kindoto. Aidha , waandishi husika hutumia visasili na hekaya kutimiza malengo yao (Wardhaugh, 1986).

Katika utafiti huu, sifa zilizoangaziwa katika utambulishaji wa kuwepo kwa uhalisiajabu ukiwa kitengo kimoja cha usasaleo na kama zilivyobainika katika utafiti wa Walibora (2010) ni pamoja na:

a. Matumizi ya wahusika wasio wa kawaida;
b. Kuwepo kwa matukio ya kiajabu;
c. Kukiukwa kwa mipaka ya kimandhari;
d. Kuwepo kwa hali za kushangaza na kuogofya;
e. Kuwepo kwa matukio ya kindoto na kifantasia;
f. Katika kazi za uhalisiajabu wakati hausongi; na
g. Hakuna mpaka wowote kati ya yanayowezekana na yasiyowezekana.

Simulizi fupi yenye urejeleomatini wa hadithi ya Shakespeare inayohusu haradali imetumika katika riwaya ili kuelezea ukweli huu. Haradali ni mbegu ndogo sana ambayo inapopandwa na kuota huchukua muda mrefu kukua lakini baadaye huwa mti mkubwa. Mti huo unapozaa, mbegu zake hutumika kukipa chakula ladha nzuri. Aidha, mti huo huwa makao ya ndege wengi. Haradali ya ubunifu imetumika kuashiria subira katika utunzi bunifu ambao matokeo yake huwafaidi wote, msomaji na mchapishaji wakiwemo. Kwa mujibu wa riwaya teule, mtunzi hutumia mambo madogomadogo katika jamii ambayo mara nyingi huanza kama uvumi ili kujenga ubunifu wake. Hatimaye subira na ukomavu huzaliwa.

Kwamba katika kiini cha kimbunga cha uvumi kuna haradali ya ubunifu. Ni kama kilele cha wimbi ambacho alisema Shakespeare kuwa kuna ufanisi.

**Mwingilianotanzu:-**

Istilahi "mwingiliano-tanzu katika fasihi hurejelea uumbaji wa maana kamili ya utanzu kutokana na utanzu mwingine. Kazi za fasihi zenye sifa ya mwingiliano-tanzu huvunja mipaka na kuchangikana wakati wa utendaji wake. Kipengele hiki kimetumiwa katika riwaya za kimajaribio kumwezesha mwandishi kutimiza wajibu wake wa kuichora sura kamili ya jamii yake. Hivyo, mwingiliano-tanzu hubainisha jinsi utanzu fulani wa fasihi unavyotagusana na tanzu nyingine na matini yote kwa jumla ili kuboresha uwasilishaji wa ujumbe (Wanjala, 2015). Katika fasihi hakuna utanzu wowote unaojitosheleza. Tanzu huingiliana ili kufaulisha uwasilishaji wa ujumbe (Mulokozi, 1996). Nadharia ya mwingiliano-tanzu kama inavyofafanuliwa na Wanjala (2015) inabaini kuwa kazi ya fasihi huumbwa kwa kuvunja mipaka ya kitanzu kwa minajili ya kutoa kazi bora zaidi kuliko ya awali. Badala ya kutumia mwandishi wa riwaya ya kisasa kutumia mtindo mmoja uliozoeleka katika usimulizi, riwaya za kimajaribio huchanganya mtindo kwa kuingiza tanzu nyingine za fasihi. Mfano;

"Jana yao ifariki – kabisaaa! Lazima unafsi wao ufe; ili umoja wao uzaliwe. Mbegu lazima ife ndipo mche uweze kuota. Kifo lazima kitangulie mapenzi au hata mapenzi yawe chanzo cha kifo kama ilivyotokea zamani. Yesu alikufa kwa kuwapenda wenye dhambi; kifo chake kikawa mwanzo wa mapenzi – bila kifo hakuna mapenzi. Hakunaaa!"

Katika simulizi hii, riwaya zimetumia kipengele cha mwingilianotanzu kuwasilishia ujumbe wake. Masimulizi yamekatizwa na kipengele cha ngano kinachopachikwa katika simulizi kuu kuendeleza hoja kwamba "kifo" kilichokithiri katika jamii ya sasa kinaweza tu kuangamizwa na jamii yenyewe. Suluhu la jamii ni jamii. Ili kubainisha taswira ya jamii ya sasa hadithi (ngano) iliyosikika kanisani wakati wa sherehe ya arusi ilirejelewa. Hadithi husika ni kifaa muhimu cha kuijuza jamii kwamba ili kupiga hatua kimaendeleo na kuimarisha huduma kwa wanajamii wote ni sharti kila mmoja afishe makosa ya kihistoria na kuyazika katika kaburi la sahau. Maneno katika katika usimulizi yalisemwa na mhubiri kwa bwana na bibi arusi. Alikuwa akiwapa wosia kwamba iwapo watapenda kuishi vizuri katika maisha ya ndoa itawabidi wafishe "jana yao". Jana inaashiria wakati uliopita. Mhubiri alisistiza kuwa ni lazima ya kale miongoni mwao kama ubinafsi yafe ili umoja wao uzaliwe. "Ni lazima mbegu ife ili mche uote". Isitoshe, kifo hutangulia mapenzi kama ilivyokuwa katika kisa cha Yesu Masihi. Ilibidi afe msalabani ili wenye dhambi wapokee msamaha kwa mujibu wa dini ya Kikristo. Kwa hivyo, kifo chake kilikuwa chanzo cha mapenzi kwa wenye dhambi. Kwa mujibu wa haya jamii ya kisasa inawajibika katika kufisha historia yake hasi ili maendeleo yapate kuota. Ukosefu wa huduma bora ni mambo yanayozalishwa na ukoloni mamboleo ambao ni zao la historia. Kitendo cha "kufisha historia" ndiko kuzaliwa kwa mara ya pili. Hivyo, taswira ya jamii ya sasa ni kwamba kutakuwa na kizazi kipya au tumaini jipya la jamii. Jamii mpya hiyo itakuwa ile iliyosahau jana yake kwa kufisha hali hasi zilizoikumba na kuzingatia mienendo mipya kwa lengo la kuinufaisha kama wasemavyo wahenga "yaliyopita si ndwele tugange yajayo."

**Hitimisho na Mapendekezo:-**

Mapendekezo ya utafiti huu yametolewa kwa makundi mawili ya washikadau wa taaluma ya fasihi. Kwanza ni kwa wasomaji (wapokeaji wote wa fasihi wakiwemo wanafunzi) na waandishi chipukizi wa riwaya za kisasa. Pili, kwa wasomi na watafiti wa baadaye wa riwaya za kimajaribio na kwa jumla kazi za fasihi za kisasa. Utafiti huu ni sehemu moja tu katika ufahamu wa utunzi wa kisasa kwa kuangazia matumizi ya mbinu za kimajaribio kama kunga za ubunifu katika riwaya mpya. Maneno mbali mbali ya waandishi kutoka kwenye riwaya husika yamemwongoza mtafiti kuafikia mapendekezo yafuatayo:

a. Wanaobuni sera za elimu na hasa katika uwanda wa elimu ya fasihi hawana budi kutoa mwanga zaidi kuhusu utunzi wa kimajaribio. Aidha, wale wanaoamua vitabu vya fasihi vinavyotahiniwa katika shule za upili hawana budi kushirikisha swala la uchanganuzi wa mbinu za kimajaribio katika mtalaa wa fasihi;

b. Wasomaji wa fasihi ya kisasa wanahimizwa kujihami na ufahamu wa kiada wa maswala mengi ya kihistoria, kidini, kijamii na kitaaluma ili waelewe au wafahamikiwe na riwaya za kimajaribio; na
c. Waandishi chipukizi hawana budi kufanya utafiti kuhusu utunzi wa kimajaribio na kufahamu njia mwafaka zaidi ya kuzitumia mbinu husika katika uandishi bunifu bila kuikanganya hadhira.

## Marejeleo:-


1. Abrams, M.H. (1993). The Norton Anthology to English Literature II. New York na London: W.W. Norton.
2. Abrams, M.H. (1999). A Glossary of Literary Terms. Ithaca: Cornell University Press.
3. Anderson, S.L. (2000). On Kierkegard. Belmont: Wadsworth/Thompson Learning Inc.
4. Bakhtin, M.M. (1981). The Dialogic Imagination: Four Essays by M.M. Bakhtin. London:
5. University of Texas Press.
6. Barth, J. (1984). “The Literature of Exhaustion” in The Friday Book: Essays and Other Non-Fiction. London: The John Hopkins University.
7. Creswell, J. W. (2009). Research design: Qualitative, quantitative, and Mixed methods Approaches. Los Angeles: Sage.
8. Chiraghdin, S. na Mnayampala, M. (1977). Historia ya Kiswahili. Nairobi: Oxford University Press.
9. Dalen, D.B.V. (1979). Understanding Education Research. London: Mc Graw-Hill.
10. Deleuze, G., na Guattari, F. (1986). Kafka: Towards a Minor Literature. Minneapolis: University of Minnesota Press.
11. Elliot, P. (2017). A Review of Z213:Exit by Dimitris Lyacos. Compulsive Reader. http://www.compulsivereader.com/2017/08/16/a-review-of-z213-exit-poena-damni-dimitris-lyacos. Tarehe ya kuingia: 25.03.2017
12. Enani, M. M. (2005). Theories of Comparative Literature. Cairo: Cairo University.
13. Faris, W.B. na Zamora, L.P. (1995). Magical Realism: Theory, History, Community. Durham: Duke University Press.
14. Frye, N., Knights, L.C. na Slote, K. (1993). Myth and Symbol: Critical Approaches and Applications. Lincoln: University of Nebraska Press.
15. Gromov, M.D. (1998). “Nagona and Mzingile- Novel, Tale or Parable?” Afrikanistische Arbeitspapiere.Swahili Forum: (55) 73–78.
16. Jazdzewska, K., (2015). “From Dialogos to Dialogue: The Use of the Term from Plato to the Second Century CE”. Greek, Roman and Byzantine Studies 54.1 pp. 17-36.
17. Karanja, M.W. (2014). Matumizi ya Istiari, Tashbiha na Taashira katika Diwani ya Sauti ya Dhiki. Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
18. Khamis, S.A.M. (1998). “Implication as a Literary Technique in Mohamed S. Mohamed’s Novels: Kiu and Nyota ya Rehema”.www.qucosa.de>qucosa>5_08khamis. Tarehe ya kuingia; 28.04.2017.
19. Kneppert, W., na Deckard, S. (2016). “Towards a Radical World Literature: Experimental Writing in a Globalizing World in A Review of International English Literature, 47 (1-2), 1-25.
20. Kristeva, J. (1980). Word, Dialogue and Novel. In Roudiez L. S. (Ed.), Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art (pp. 64-91). New York, NY: Colombia University Press.
21. Leech, G.N., (1969). A Linguistic Guide to English Poetry. London: Longman.
22. Lyotard, J.F. (1984). The Postmodern Condition: A Report on Knowledge. Translated by Bennington, G na Massumi, B. Minneapolis: University of Minnesota Press.
23. Maree, J. G. (Ed.), (2012) Complete your Thesis or Dissertation Successfully: Practical Guidelines. Cape Town: Juta.
24. Martha, C. (2008). “On the Work of Italo Calvino”, The Writers Chronicle 24-32.
25. Mbatiah (2001b).Kamusi ya Fasihi. Nairobi: Standard Textbooks and Graphics Publishers.
26. Mugenda, O.M. na Mugenda, A.G., (2003).Research Methods, Quantitative and Qualitative Approaches. Nairobi: ACT.
27. Mulokozi, M., (1996).Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.
28. Musokile, M., (1993).Misingi ya Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: East African Educational
29. Publishers.
30. Mwakio, L.W. (2014). Matumizi ya Tashbiha, Sitiari na Taashira katika Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine. Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi.
31. Mwamzandi, I.Y., (2013). “Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia ya Fasihi”. Swahili Forum, (20), 48-66.
32. Myers, J. na Simms, M. (1989). The Longman Dictionary of Poetic Terms. New York: Longman.

33. Neuendorf, K.A. (2002). The Content Analysis Handbook. Thousand Oaks: Sage.
34. Pakenham, T. (1992). The Scramble for Africa: Whitman's Conquest of the Dark Continent from 1876-1912. New York: Avon.
35. Rettova, A. (2016). "Writing in the Swing? Neo-realism in Post- Experimental Swahili Fiction". Research in African Literatures, (47) 2 15-31.
36. Richards, J.C. (1984). Error Analysis Persepectives on Second Language. London: Longman Group Ltd.
37. Senkoro, F.E.M.K. (1982). Fasihi. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
38. Stam, R. (2000). Film Theory: An Introduction. Oxford: Blackwell.
39. Walibora, K. (2010). Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum. Swahili Forum.
40. Wamitila, K.W. (2004). Musaleo! Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
41. Wamitila, K.W. 2011). Msichana wa Mbalamwezi. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
42. Wamitila, K.W. (2014). Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
43. Wamitila, K.W. (2010). Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.
44. Wanjala, W.F. (2015). Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa. Tasnifu ya Uzamifu; Chuo Kikuu cha Kenyatta.
45. Wardhaugh, R. (1986). An Introduction to Socio-Linguistics. New York: Blackwell Publishers.
46. William, H. (2003). A Hand Book to Literature. 9th Edition. Upper Saddle River, New Jersey: Prentice Hall.
47. Zabus, C. (1997). Postmodernism in African Literature in English.
48. https://www.researchgate.net/publication/300837404 doi:10.1075/chlel.xi.59zab
49. Tarehe ya kuingia; 01.05.2017.